RISING STAR EXAMINATION SERIES

# DARASA LA TANO

**MWAKA WA 2021**

## KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

Dedicated to Excellence

Muda: Saa 1 dakika 40

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU***

1. Tumia penseli ya kawaida tu.
2. Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:-
   *(i) JINA LAKO* *(ii) JINA LA SHULE YAKO*
3. Kwa kila swali onyesha kwa kupiga mstari kwenye mabano lile jibu ulilolichagua limeandikwa.

***Soma kifungu kifuatacho kisha uchague jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa ili kujaza nafasi 1-15.***

Hapo __1__ za kale paka __2__ kufanya __3__ na chui kwani __4__ kuwa chui __5__ na wanyama __6__ wa mwituni __7__ ya ukali wake. Siku moja wakiwa mawindoni wapate kitu cha __8__, __9__ na twiga.

Twiga ni mnyama __10__ shingo __11__ ajabu, lakini chui __12__ bali __13__ twiga kwenye shingo __14__ akitaka __15__ ili wapate mlo wa siku hiyo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. samani | B. zamani | C. shamani | D. thamani |
| 2. | A. aliamua | B. alipendekeza | C. alilia | D. akitaka |
| 3. | A. marafiki | B. rafiki | C. virafiki | D. urafiki |
| 4. | A. alidhani | B. alipenda | C. alithani | D. alitamani |
| 5. | A. haogopwi | B. ogopea | C. aliogopwa | D. aliogope |
| 6. | A. zote | B. wote | C. yote | D. kote |
| 7. | A. kwa sababu | B. maana | C. kwasababu | D. mbali |
| 8. | A. kukula | B. kulia | C. chakula | D. kula |
| 9. | A. walipitana | B. walikutana | C. walilia | D. walikuta |
| 10. | A. aliye | B. ambaye | C. mwenye | D. akaona |
| 11. | A. ndefu | B. mrefu | C. refu | D. lirefu |
| 12. | A. aliogopa | B. hakuogopwa | C. waliogopa | D. hakumwogopa |
| 13. | A. aliirukia | B. alimrukia | C. aliuruka | D. aliruka |
| 14. | A. yake | B. mwake | C. lake | D. zake |
| 15. | A. kumuua | B. kumla | C. kuuwala | D. kuua |



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Kutoka swali la 16-30, jibu kwa kufuata maagizo***

**16.** Mtu akikwambia pole utamjibu _______

A. sawa

B. asante

C. nimeshapoa

D. njema

**17.** ***Jaza pengo kwa kutumia kiulizi pi ipasavyo.***

Ni kitabu _______ utasoma?

A. yupi B. vipi

C. kipi D. zipi

**18.** Tandiko la sakafuni ni ________

A. zulia B. takia

C. kochi D. shubaka

**19.** Chagua vazi linalovaliwa na wanaume pekee?

A. Sindiria B. Shimizi

C. Gauni D. Shati

**20.** Je, akisami $^1/_6$ huitwaje?

A. Sudusi B. Robo

C. Tusui D. Subui

**21.** Kitanda ambacho hutumiwa kubebea mgonjwa huitwa:-

A. ambulensi B. machela

C. kidonge D. kitata

**22.** Mmea ambao zao lake linatengeneza dawa za kuwaua wadudu ni:-

A. mshayiri B. mpareto

C. mgomba D. mnazi

**23.** Kifungu kimoja cha shairi huitwa _______

A. kina B. mizani

C. kibwagizo D. ubeti

**24.** ***Kanusha:*** Miti imeanguka.

A. Miti haikuanguka

B. Miti hayajaanguka

C. Miti haijaanguka

D. Miti haianguki

**25.** ***Kamilisha methali.***

_______ ya mbali haiui nyoka,

A. Bunduki B. Jiwe

C. Fimbo D. Risasi

**26.** ***Andika kwa wingi***

Kiti hiki ni changu.

A. Viti hivi ni vyangu.

B. Viti hivi ni vyetu

C. Viti hivi ni zetu

D. Viti hivi ni vyenu

**27.** Ni sentensi ipi iko katika wakati ujao?


A. Mimi ninakula chakula

B. Wewe umekunywa chai

C. Yeye atasafiri mjini.

D. Nyinyi mlipita mtihani

**28.** Umbo hili huitwa ________



A. mstatili B. duara

C. mche D. mraba

**29.** Fundi wa mbao huitwa _______

A. mhunzi

B. mwashi

C. dobi

D. seremala

**30.** Asubuhi jua huchomoza upande wa _________

A. Magharibi

B. Kusini

C. Mashariki

D. Kaskazini



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.***

Hapo zamani za kale chawa na nyigu walipanga kuhudhuria sherehe. Kabla ya sherehe walionelea ni bora waoge na kujitakasa vizuri. Kwa vile hawakutaka kujipangusa kwa taulo, walijianika juani ili wakauke.

Baada ya kupumzika juani, walionelea ni heri wavae ili wasichelewe kuhudhuria sherehe. Wote walikuwa na sime. Nyigu akamwambia rafiki yake chawa amsaidie kuifunga sime yake kiunoni. Chawa akaifunga kwa nguvu karibu kukikata kiuno cha nyigu. Alipoona wembamba wa kiuno cha mwenzake chawa alianza kucheka. Alicheka akacheka hadi pua yake ikapasuka. Tangu siku hiyo, kiuno cha nyigu kikawa chembamba nayo pua ya chawa ikawa imepasuka.

**31.** Chawa na nyigu walipanga kufanya nini?

A. Kwenda safari

B. Kula nyama

C. Kuhudhuria sherehe

D. Kujipangusa uso

**32.** Nyigu na chawa ni aina ya ________

A. wadudu

B. nyuni

C. wanyama

D. samaki

**33.** ***Kamilisha methali:***

Kidole kimoja hakivunji ________

A. mdudu

B. nyigu

C. chawa

D. punje

**34.** Sime ni aina ya ________

A. mshipi

B. kisu

C. bangili

D. simu

**35.** Ni nini maana ya neno **takasa** kama lilivyotumiwa katika kisa hiki?

A. Ringa B. Ogofya

C. Danganya D. Safisha

**36.** Kwa nini chawa alicheka sana?

A. Nyigu alipocheka

B. Kwa kushiba

C. Alipoona wembamba wa kiuno cha nyigu

D. Alifurahishwa na maji

**37.** Neno jingine lenye maana sawa na "sherehe" ni __

A. sikukuu

B. karamu

C. chakula

D. furaha

**38.** Kwa nini chawa alipasuka pua?

A. Alicheka sana

B. Aligongwa kwa mawe

C. Alikatwa na nyigu

D. Alijikata

**39.** Rafiki ni yule ________

A. jirani

B. anayekupa zawadi

C. anayekusaidia wakati wa shida

D. wa ukoo wenu

**40.** Kichwa mwafaka cha kisa hiki ni:-

A. Kupasuka pua kwa chawa

B. Chawa na nyigu

C. Sherehe ya nyigu

D. Nyigu na sime



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50.***

**Shule ya msingi ya Johari,**
**S.L.P 9227,**
**Madongoporomoka**
**9-6-2017**

**Rafiki mpendwa Chausiku,**

Hujambo? Vipi huku kwenu? Ndugu zako hawajambo? Habari za wazazi? Bila shaka wote wazima.

Baada ya salamu nataka kukujulisha kwamba ninaendelea vizuri na masomo yangu. Wazazi wangu, baba na mama wote ni wazima na wako salama salimini.

Lengo la barua yangu ni kukujulisha kuwa mama ameninunulia tuzo ya mwanasesere mzuri sana. Ukipata nafasi njoo kwetu siku ya Jumapili tucheze pamoja. Pia, baba ameninunulia baiskeli kama ile yako. Uje na baiskeli yako tucheze pamoja.

Ninafuraha kukwambia tulifanya mtihani muhula uliopita. Nilikuwa nambari mbili. Nilipita vizuri sana. Nilifurahi. Mwalimu wetu wa darasa alinipa zawadi. Nilipewa kalamu mbili za risasi, madaftari matatu, kitabu cha hadithi na kamusi ya Kiswahili sanifu.

Mwisho nakuombea baraka za Mungu.

**Ni mimi rafiki yako,**
**Pendo Zuzu**

---

**41.** Mwandishi wa barua hii anasomea shule ipi?
A. Teko  B. Johari
C. Kibe  D. Baria

**42.** Mwandishi anaishi karibu na mji wa:-
A. Kagumo  B. Bewa
C. Madongoporomoka  D. Pewa

**43.** Hii ni barua ya aina gani?
A. Rasmi  B. Wazazi
C. Utamaduni  D. Kirafiki

**44.** Jina jingine la tuzo ni ______
A. zawadi  B. pesa
C. barua  D. kitabu

**45.** Mwandishi alinunuliwa **tuzo** gani na mamake?
A. Kamusi  B. Kalamu ya risasi
C. Mwanasesere  D. Viatu

**46.** Barua hii iliandikwa mwaka gani?
A. 2015  B. 2013
C. 2017  D. 2016

**47.** Mwandishi wa barua hii ni nani?
A. Pendo Zuzu
B. Chausiku
C. Madongoporomoka
D. Mwalimu

**48.** Chausiku aliambiwa aende siku gani wacheze pamoja?
A. Jumamosi
B. Jumapili
C. Jumatatu
D. Ijumaa

**49.** Maana ya S.L.P ni ______
A. Sanduku La Posta
B. Safari Ya Petro
C. Samaki La Posta
D. Simu La Posta

**50.** Barua hii ina anwani ngapi?
A. 4  B. 2  C. 1  D. 0



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com